BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Tano – Tarehe 25 Septemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2017/2018.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2017/2018.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

144. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Viongozi wa Mataifa mbalimbali walipokuwa wakifanya ziara Tanzania, walikuwa wakifika na Zanzibar. Hata hivyo, katika siku za hivi karibuni wanaishia Tanzania Bara wakati utaratibu wa zamani unaonekana kuwa na umuhimu mkubwa kwa Zanzibar kuimarisha ushirikiano wa kisiasa na kiuchumi.

(a) Je, sababu gani viongozi hao wamekuwa wakiishia Tanzania Bara na Viongozi wa Zanzibar kulazimika wakati mwengine kwenda Tanzania Bara kinyume na utaratibu wa siku za nyuma.

(b) Je, ni Viongozi wangapi wa Kitaifa waliofanya ziara ya kuitembelea Tanzania bila ya kufika Zanzibar tangu mwaka 2015.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

148. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Baraza la Manispaa Mjini lina wafanyakazi wangapi wote kwa jumla ukianzia Meya na Mkurugenzi wake.

(a) Kitengo cha usafishaji barabara kina wafanyakazi wangapi na wanaanza kazi saa ngapi na kumaliza saa ngapi.

(b) Je, ni nini kazi za Manispaa ili wananchi wapate kujua.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

23. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa kuna tatizo kubwa la wanafunzi kwenye skuli ya Konde Msingi “A” na “B” jambo lililosababishwa na uchache wa madarasa na pia kuvunjwa kwa madarasa kutokana na uchakavu ambapo hadi leo bado hayajajengwa.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kujenga madarasa mengine ili kusaidia kupunguza mrundikano mkubwa wa wanafunzi kwenye madarasa ambapo kwa sasa kila darasa linabeba zaidi ya wanafunzi themanini (80).

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa haraka ili kuliondoa tatizo la madarasa sambamba na tatizo la vyoo ukizingatia kwamba skuli hiyo ipo katikati ya mji na ina idadi kubwa ya wanafunzi.

76. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Maji ni huduma muhimu kwa maisha ya binaadamu, lakini bado huduma hiyo haipatikani katika Skuli ya Mtule na kuathiri shughuli za masomo katika skuli hiyo.

Je, juhudi gani za haraka zimechukuliwa kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwa uhakika katika skuli hiyo.

.

Wizara ya Afya:

119. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na jitihada za Serikali katika udhibiti na ukaguzi mzuri wa chakula, dawa na vipodozi lakini bado kuna malalamiko mengi ya vyakula, dawa na vipodozi ama kuwa feki au kupitwa na muda na taarifa zake kuorodheshwa kwenye mitandao ya kijamii. Hata hivyo Wizara hunyamaza kimya bila ya kuthibitisha au kukanusha taarifa hizo.

(a) Je, Wizara hawayaoni hayo.

(b) Je, Wizara haina kitengo cha habari ambacho kinajibu taarifa hizo au kitengo cha sheria kinachodhibiti kutolewa kwa taarifa hizo.

(c) Je, Wizara haioni kunyamaza kunaweza kuleta taharuki na athati kwa wananchi wake.

Wizara ya Fedha na Mipango:

54. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kampuni ya CRJE imejenga majengo mengi hapa Zanzibar yakiwemo Chawl Building, Wizara ya Katiba na Sheria na Michenzani (Mapinduzi Square) na mengine ambapo pia kuna matarajio mengine ya kazi kupewa Kampuni hiyo.

(a) Je, hapa Zanzibar hakuna Kampuni za Wazawa mpaka kazi hizo kupewa Kampuni ya Kigeni.

(b) Je, ni sababu gani zilizoelekeza Kampuni hiyo kupewa kazi nyingi na huku tukijua ujenzi wake ni ghali na mara kwa mara husaini mikataba njiani.

(c) Je, ni nani anaesimamia zabuni (tender) hizo na huziwekea vigezo vipi.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

57. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa Serikali ilishakubali kuanza na kuendeleza maonyesho ya kilimo na wajasiriamali Zanzibar na kuweka tarehe 8/8 ya kila mwaka kwa Unguja na 16/10 ya kila mwaka kwa upande wa Pemba.

(a) Je, maeneo gani yaliyowekwa kwa upande wa Pemba.

(b) Je, hatua gani iliyochukuliwa ya matayarisho na kuimarisha maonyesho hayo.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

108. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua jitihada kubwa katika usambazaji wa umeme mijini na vijijini pamoja na visiwa vyengine vidogo vidogo vilivyopo Zanzibar. Pamoja na jitihada hizo, kuna kijiji kipya kinachotoka Muharitani - Chake/Michakaini - Chake hadi Pagali kupitia Ngomahazingwa, ambacho mpaka sasa hakina umeme.

(a) Je, Serikali inakitambua kijiji hicho, kilichopo mjini na hakina umeme.

(b) Je, ni lini watapeleka umeme katika kijiji hicho.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

124. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kumekuwa na tatizo la kuzuiliwa kupitisha "Body Spray" katika kiwanja cha ndege cha Pemba sambamba na kuharibika mara kwa mara mashine za ukaguzi wa mizigo

jambo linalosababisha wafanyakazi kupekuwa mizigo kwa mikono na kusababisha usumbufu kwa abiria hao.

(a) Je, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ina mpango gani wa kununua mashine nyengine mpya za kukagulia mizigo sambamba na kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara mashine kongwe zilizopo ili kuimarisha utendaji kazi na kuondoa usumbufu kwa wasafiri wanaotumia viwanja vyetu vya ndege.

(b) Je, kuna sababu gani ya msingi iliyopelekea viwanja vya Kimataifa kama vile JK. Nyerere na Abeid Amani Karume vikaruhusiwa kupitisha "Body Spray" lakini wasafiri wa kupitia kiwanja cha Pemba wakazuiliwa

III. HOJA ZA SERIKALI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2017/2018.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa mwaka 2017/2018.

Zanzibar, **(Raya Issa Msellem)**
25 Septemba, 2018. **KATIBU WA BARAZA.**